JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Ripoti ya Takwimu za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi

## Matokeo Muhimu



MATOKEO YA SENSA YA SITA
TANZANIA
SENSA
2022
MIPANGO JUMUISHI KWA MAENDELEO ENDELEVU

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Ripoti ya Takwimu za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi

## Matokeo Muhimu

Wizara ya Fedha
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanzania

na

Ofisi ya Rais,
Wizara ya Fedha na Mipango
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Zanzibar

**Aprili, 2024**

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyokuwa kwa awamu zilizotangulia, ilitimiza wajibu wake wa kufanya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022 (SWM 2022). Sensa zilizotangulia ambazo zilifanyika baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Tarehe rejea kwa ajili ya SWM ya 2022 ilikuwa ni usiku wa tarehe 22 kuamkia 23 Agosti 2022 na ilifanyika kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura Na. 351 ambayo inaielekeza Serikali kufanya Sensa ya Watu na Makazi kila baada ya miaka kumi. Tofauti na Sensa zilizotangulia, Sensa ya mwaka 2022 ni ya kwanza kufanyika kidijitali Tanzania katika hatua zote za utekelezaji.

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 pamoja na taarifa zingine, ilikusanya taarifa za kidemografia, shughuli za kiuchumi, hali ya ulemavu, uhamaji/uhamiaji na upatikanaji wa huduma za kijamii.  Matokeo ya Sensa huiwezesha Serikali na wadau wa maendeleo kusimamia na kutathmini mipango ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa mwaka 2050; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/2022 – 2025/26; na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021/22 - 2025/26; Mpango wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Mpango wa Maendeleo wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika 2050; na Ajenda ya Afrika 2063.

Kijitabu hiki kinatoa muhtasari wa matokeo muhimu ya viashiria vya msingi kutokana na Ripoti ya Takwimu za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kila ilipowezekana taarifa za Sensa ya mwaka 2022 zimelinganishwa na za Sensa ya Mwaka 2012 ili kuangalia mabadiliko kwa kipindi husika na kupata mwelekeo wa viashiria. Viashiria vimetolewa kijinsi kila ilipowezekana.

Mada zilizopo kwenye kijitabu hiki ni pamoja na idadi ya watu; ongezeko la idadi ya watu; mgawanyo wa watu kwa umri na jinsi; muundo wa kaya; hali ya ndoa; uraia na nyaraka za utambulisho. Mada nyingine ni hali ya uyatima, elimu, shughuli za kiuchumi, ulemavu, umiliki wa ardhi, hali ya makazi, umiliki wa vifaa na udhibiti wa mazingira; pamoja na upatikanaji na matumizi ya vifaa vya mawasiliano

**Muhtasari wa Matokeo Muhimu ya Takwimu za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi; Tanzania, SWM 2022**

| Kiashiria | Tanzania | | Tanzania Bara | | Tanzania Zanzibar | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia |
| **Idadi, Ongezeko na Mgawanyo wa Idadi ya Watu** | | | | | | |
| Idadi ya Watu | **61,741,120** | **100.0** | **59,851,347** | **100.0** | **1,889,773** | **100.0** |
| Wanaume | 30,053,130 | 48.7 | 29,137,638 | 48.7 | 915,492 | 48.4 |
| Wanawake | 31,687,990 | 51.3 | 30,713,709 | 51.3 | 974,281 | 51.6 |
| Kijijini | 40,201,425 | 65.1 | 39,237,927 | 65.6 | 963,498 | 51.0 |
| Mjini | 21,539,695 | 34.9 | 20,613,420 | 34.4 | 926,275 | 49.0 |
| Wastani wa Kasi ya Ongezeko la Idadi ya Watu kwa Mwaka (2012 - 2022) | - | 3.2 | - | 3.2 | - | 3.7 |
| **Makundi ya Umri na Jinsi** | | | | | | |
| Watoto (Miaka 0 – 4) | **9,484,171** | **15.4** | **9,207,432** | **15.4** | **276,739** | **14.6** |
| Wanaume | 4,723,359 | 15.7 | 4,584,972 | 15.7 | 138,387 | 15.1 |
| Wanawake | 4,760,812 | 15.0 | 4,622,460 | 15.1 | 138,352 | 14.2 |
| Idadi ya Watoto (Miaka 0 – 14) | **26,399,988** | **42.8** | **25,628,380** | **42.8** | **771,608** | **40.8** |
| Wanaume | 13,193,149 | 43.9 | 12,807,157 | 44.0 | 385,992 | 42.2 |
| Wanawake | 13,206,839 | 41.7 | 12,821,223 | 41.7 | 385,616 | 39.6 |
| Idadi ya Watoto (Miaka 0 – 17) | **30,257,196** | **49.0** | **29,365,234** | **49.1** | **891,962** | **47.2** |
| Wanaume | 15,128,975 | 50.3 | 14,684,339 | 50.4 | 444,636 | 48.6 |
| Wanawake | 15,128,221 | 47.7 | 14,680,895 | 47.8 | 447,326 | 45.9 |
| Idadi ya Vijana (Miaka 15 – 24) | **11,848,365** | **19.2** | **11,463,718** | **19.2** | **384,647** | **20.4** |
| Wanaume | 5,657,379 | 18.8 | 5,474,799 | 18.8 | 182,580 | 19.9 |
| Wanawake | 6,190,986 | 19.5 | 5,988,919 | 19.5 | 202,067 | 20.7 |
| Idadi ya Vijana (Miaka 15 – 35) | **21,312,411** | **34.5** | **20,612,566** | **34.4** | **699,845** | **37.0** |
| Wanaume | 10,159,205 | 33.8 | 9,827,426 | 33.7 | 331,779 | 36.2 |
| Wanawake | 11,153,206 | 35.2 | 10,785,140 | 35.1 | 368,066 | 37.8 |
| Wanawake wenye Umri wa Kuzaa (Miaka 15 - 49) | **14,992,288** | **47.3** | **14,501,431** | **47.2** | **490,857** | **50.4** |
| Nguvu Kazi (Miaka 15 - 64) | **33,000,224** | **53.4** | **31,936,653** | **53.4** | **1,063,571** | **56.3** |
| Wanaume | 15,828,450 | 52.7 | 15,323,862 | 52.6 | 504,588 | 55.1 |
| Wanawake | 17,171,774 | 54.2 | 16,612,791 | 54.1 | 558,983 | 57.4 |

| Kiashiria | Tanzania | | Tanzania Bara | | Tanzania Zanzibar | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia |
| Idadi ya Wazee (Miaka 60+) | **3,491,983** | **5.7** | **3,406,465** | **5.7** | **85,518** | **4.5** |
| Wanaume | 1,586,759 | 5.3 | 1,546,222 | 5.3 | 40,537 | 4.4 |
| Wanawake | 1,905,224 | 6.0 | 1,860,243 | 6.1 | 44,981 | 4.6 |
| Idadi ya Wazee (Miaka 65+) | **2,340,908** | **3.8** | **2,286,314** | **3.8** | **54,594** | **2.9** |
| Wanaume | 1,031,531 | 3.4 | 1,006,619 | 3.5 | 24,912 | 2.7 |
| Wanawake | 1,309,377 | 4.1 | 1,279,695 | 4.2 | 29,682 | 3.0 |
| **Muundo wa Kaya** | | | | | | |
| Idadi ya Kaya Binafsi | 14,152,803 | 100.0 | 13,776,975 | 100.0 | 375,828 | 100.0 |
| Kijijini | 8,547,333 | 60.4 | 8,355,992 | 60.7 | 191,341 | 50.9 |
| Mjini | 5,605,470 | 39.6 | 5,420,983 | 39.3 | 184,487 | 49.1 |
| Kaya Zinazoongozwa na Wanaume | 9,088,599 | 64.2 | 8,828,073 | 64.1 | 260,526 | 69.3 |
| Kaya Zinazoongozwa na Wanawake | 5,064,204 | 35.8 | 4,948,902 | 35.9 | 115,302 | 30.7 |
| Wastani wa Watu katika Kaya[1] | - | 4.3 | - | 4.3 | - | 4.9 |
| Zinazoongozwa na Wanaume | - | 4.4 | - | 4.4 | - | 5.0 |
| Zinazoongozwa na Wanawake | - | 4.0 | - | 4.0 | - | 4.8 |
| **Hali ya Ndoa (Miaka 15 na zaidi)** | | | | | | |
| Hawajawahi Kuoa au Kuolewa | 11,644,757 | 32.9 | 11,239,622 | 32.8 | 405,135 | 36.2 |
| Waliooa au Kuolewa | 18,168,489 | 51.4 | 17,563,702 | 51.3 | 604,787 | 54.1 |
| Wanaishi Pamoja | 1,928,364 | 5.5 | 1,920,758 | 5.6 | 7,606 | 0.7 |
| Wametengana | 631,491 | 1.8 | 626,732 | 1.8 | 4,759 | 0.4 |
| Wameachana | 1,291,438 | 3.7 | 1,228,869 | 3.6 | 62,569 | 5.6 |
| Wajane | 1,676,592 | 4.7 | 1,643,283 | 4.8 | 33,309 | 3.0 |
| **Wastani wa Umri wa Kuoa au Kuolewa kwa mara ya Kwanza[2]** | | | | | | |
| Wanaume | 26.4 | - | 26.3 | - | 27.8 | - |
| Wanawake | 22.1 | - | 22.1 | - | 23.7 | - |
| **Nyaraka za Kitaifa za Utambulisho na Uraia** | | | | | | |

[1] Namba hizi ni wastani na sio asilimia

[2] Wastani wa umri na sio asilimia

| Kiashiria | Tanzania | | Tanzania Bara | | Tanzania Zanzibar | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia |
| **Usajili wa Vizazi** | | | | | | |
| Watu wenye Vyeti vya Kuzaliwa | 17,466,823 | 28.8 | 16,074,723 | 27.3 | 13.92,100 | 75.1 |
| Watu wenye Tangazo la Kizazi | 1,862,537 | 3.1 | 1,782,330 | 3.0 | 80,207 | 4.3 |
| **Uraia** | | | | | | |
| Watanzania | 61,457,853 | 99.5 | 59,575,361 | 99.5 | 1,882,492 | 99.6 |
| Wasio Watanzania | 283,267 | 0.5 | 275,986 | 0.5 | 7,281 | 0.4 |
| **Hali ya Uyatima** | | | | | | |
| Yatima (Miaka 0 - 17) | 3,133,199 | 10.4 | 3,076,633 | 10.5 | 56,566 | 6.3 |
| **Kujua Kusoma na Kuandika, Kuhesabu na Elimu** | | | | | | |
| Kiwango cha Wanaojua Kusoma na Kuandika (Miaka 15 na zaidi) | 29,336,514 | 83.0 | 28,323,159 | 82.8 | 1,013,355 | 90.6 |
| Kiwango cha Wanaojua Kusoma na Kuandika kwa Vijana (Miaka15 - 24) | 10,458,013 | 88.3 | 10,087,291 | 88.0 | 370,722 | 96.4 |
| Kiwango cha Wanaojua Kusoma na Kuandika kwa Vijana (Miaka15 - 35) | 18,694,762 | 87.7 | 18,026,390 | 87.5 | 668,372 | 95.5 |
| Kiwango Halisi cha Uandikishaji Shule za Msingi **(Miaka 7 – 13)** | 9,733,049 | 83.3 | 9,400,610 | 82.9 | 332,439 | 96.9 |
| Kiwango cha Uandikishaji Shule za Msingi (Bila ya Kujali Umri) | 14,400,341 | 123.2 | 13,888,071 | 122.4 | 512,270 | 149.4 |
| Kiwango cha Kujua Kuhesabu (Numeracy Rate) | 29,206,469 | 84.7 | 28,223,190 | 84.5 | 983,279 | 90.6 |
| Kiwango cha Juu cha Elimu Kilichofikiwa (Miaka 4 na Zaidi) | | | | | | |
| **Jumla** | **26,170,109** | **100.0** | **25,325,105** | **100.0** | **845,002** | **100.0** |
| Elimu ya Msingi | 18,739,101 | 67.9 | 18,480,477 | 69.2 | 258,624 | 30.6 |
| Mafunzo Baada ya Elimu ya Msingi | 60,613 | 0.2 | 60,035 | 0.2 | 578 | 0.1 |
| Elimu ya Sekondari | 5,455,805 | 19.8 | 5,218,386 | 19.6 | 511,403 | 60.5 |
| Mafunzo Baada ya Elimu ya Sekondari | 250,795 | 0.9 | 247,056 | 0.9 | 3,739 | 0.4 |
| Chuo Kikuu na Vyuo Vingine Vinavyolingana | 1,389,809 | 5.0 | 1,319,151 | 4.9 | 70,658 | 8.4 |
| **Shughuli za Kiuchumi** | | | | | | |
| Jumla | **24,695,842** | **100.0** | **23,986,730** | **100.0** | **709,112** | **100.0** |
| Wabunge, Watawala na Mameneja | 148,340 | 0.6 | 132,561 | 0.6 | 15,779 | 2.2 |
| Wataalamu | 536,909 | 2.2 | 501,513 | 2.1 | 35,396 | 5.0 |

| Kiashiria | Tanzania | | Tanzania Bara | | Tanzania Zanzibar | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia |
| Mafundi na Wataalam Washiriki | 1,100,951 | 4.5 | 1,047,869 | 4.4 | 53,082 | 7.5 |
| Makarani | 130,585 | 0.5 | 120,074 | 0.5 | 10,511 | 1.5 |
| Watoa Huduma na Wauzaji Maduka | 1,600,236 | 6.5 | 1,514,183 | 6.3 | 86,053 | 12.1 |
| Wanaofanya Shughuli za Kilimo na Uvuvi | 10,673,599 | 43.2 | 10,501,954 | 43.8 | 171,645 | 24.2 |
| Wafanyakazi wa Kazi za Mikono na Wanaofanana nao | 4,870,084 | 19.7 | 4,735,058 | 19.7 | 135,026 | 19.0 |
| Waunganishaji na Waendeshaji wa Mashine kwenye viwanda | 286,692 | 1.2 | 278,845 | 1.2 | 7,847 | 1.1 |
| Kazi za Kawaida Zisizo na Ujuzi | 5,348,442 | 21.7 | 5,154,669 | 21.5 | 193,773 | 27.3 |
| **Ulemavu** | | | | | | |
| Kiwango cha Ulemavu | 5,347,397 | 11.2 | 5,180,095 | 11.2 | 167,302 | 11.4 |
| **Aina ya Ulemavu** | | | | | | |
| Albino | 74,273 | 0.12 | 71,631 | 0.12 | 2,642 | 0.14 |
| Kuona | 1,447,853 | 3.0 | 1,394,512 | 3.0 | 53,341 | 3.6 |
| Kusikia | 539,186 | 1.1 | 518,846 | 1.1 | 20,340 | 1.4 |
| Kutembea | 876,290 | 1.8 | 856,476 | 1.9 | 19,814 | 1.3 |
| Kukumbuka | 301,663 | 0.6 | 294,133 | 0.6 | 7,530 | 0.5 |
| Kujihudumia | 156,211 | 0.3 | 132,531 | 0.3 | 2,980 | 0.2 |
| Kuwasiliana | 291,185 | 0.6 | 285,877 | 0.6 | 5,308 | 0.4 |
| Ulemavu Mwingine | 1,755,709 | 3.7 | 1,697,720 | 3.7 | 57,989 | 3.9 |
| **Hali ya Makazi, Umiliki wa Vifaa na Udhibiti wa Mazingira** | | | | | | |
| **Hali ya Umiliki (Jengo Kuu)** | | | | | | |
| Linamilikiwa na Kaya | 9,199,208 | 65.0 | 8,930,979 | 64.8 | 268,229 | 71.4 |
| Kuishi Bila Kulipa Kodi | 831,895 | 5.9 | 787,589 | 5.7 | 44,306 | 11.8 |
| Imepangishwa Binafsi | 2,829,001 | 20.0 | 2,786,034 | 20.2 | 42,967 | 11.4 |
| Kupangishiwa na Mwajiri | 382,916 | 2.7 | 377,833 | 2.7 | 5,083 | 1.4 |
| Kupangishiwa na Serikali kwa Kodi nafuu | 424,960 | 3.0 | 417,329 | 3.0 | 7,631 | 2.0 |
| Inamilikiwa na Mwajiri – Bila Malipo | 275,474 | 1.9 | 271,347 | 2.0 | 4,127 | 1.1 |
| Inamilikiwa na Mwajiri – Kwa Malipo nafuu | 209,349 | 1.5 | 205,864 | 1.5 | 3,485 | 0.9 |
| **Vifaa Vilivyotumika Kuezekea** | | | | | | |

| Kiashiria | Tanzania | | Tanzania Bara | | Tanzania Zanzibar | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia |
| Mabati | 12,005,537 | 84.8 | 11,657,933 | 84.6 | 347,604 | 92.5 |
| Majani au Makuti | 1,639,904 | 11.6 | 1,618,376 | 11.7 | 21,528 | 5.7 |
| Matope na Majani | 343,736 | 2.4 | 343,135 | 2.5 | 601 | 0.2 |
| Aina Nyingine | 163,626 | 1.2 | 157,531 | 1.1 | 6,095.0 | 1.6 |
| **Vifaa Vilivyotumika Kusakafia** | | | | | | |
| Saruji | 6,953,852 | 49.1 | 6,668,320 | 48.4 | 285,532 | 76.0 |
| Udongo | 5,853,301 | 41.4 | 5,809,497 | 42.2 | 43,804 | 11.7 |
| Vigae/Tailizi | 1,044,625 | 7.4 | 1,001,503 | 7.3 | 43,122 | 11.5 |
| Aina Nyingine | 301,025 | 2.3 | 297,655 | 2.3 | 3,370 | 0.8 |
| **Vifaa Vilivyotumika Kujengea Kuta** | | | | | | |
| Matofali ya Saruji | 3,978,510 | 28.1 | 3,689,564 | 26.8 | 288,946 | 76.9 |
| Matofali ya Udongo ya Kuchoma | 4,878,014 | 34.5 | 4,876,451 | 35.4 | 1,563 | 0.4 |
| Matofali ya Udongo yasiyo ya Kuchoma | 2,618,579 | 18.5 | 2,612,788 | 19.0 | 5,791 | 1.5 |
| Mianzi/Miti na Udongo | 2,218,644 | 15.7 | 2,175,860 | 15.8 | 42,784 | 11.4 |
| Mawe | 169,114 | 1.2 | 135,031 | 1.0 | 34,083 | 9.1 |
| Aina Nyingine | 289,942 | 2.1 | 287,281 | 2.1 | 2,661 | 0.7 |
| **Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia** | | | | | | |
| Umeme (TANESCO/ZECO) | 5,295,412 | 37.4 | 5,043,801 | 36.6 | 251,611 | 66.9 |
| Umeme wa Mionzi ya Jua | 4,592,359 | 32.4 | 4,573,584 | 33.2 | 18,775 | 5.0 |
| Mafuta ya Taa | 559,550 | 4.0 | 482,194 | 3.5 | 77,356.0 | 20.6 |
| Aina Nyingine | 3,705,482 | 26.2 | 3,677,396 | 26.7 | 28,086 | 7.5 |
| **Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kupikia** | | | | | | |
| Kuni | 7,885,115 | 55.7 | 7,709,031 | 56.0 | 176,084 | 46.9 |
| Mkaa | 3,667,039 | 25.9 | 3,558,380 | 25.8 | 108,659 | 28.9 |
| Mafuta ya Taa | 71,288 | 0.5 | 65,095 | 0.5 | 6,193 | 1.6 |
| Umeme | 604,051 | 4.3 | 575,982 | 4.2 | 28,069 | 7.5 |
| Gesi | 1,315,037 | 9.3 | 1,266,844 | 9.2 | 48,193 | 12.8 |
| Aina Nyingine | 610,273 | 4.3 | 601,643 | 4.4 | 8,630 | 2.3 |
| **Chanzo Kikuu cha Maji ya Kunywa** | | | | | | |
| Maji ya Bomba/Mfereji | 7,200,680 | 50.9 | 6,919,926 | 50.2 | 280,754 | 74.7 |

| Kiashiria | Tanzania | | Tanzania Bara | | Tanzania Zanzibar | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia | Namba | Asilimia |
| Vyanzo Vingine Vilivyohifadhiwa | 2,718,642 | 19.2 | 2,651,465 | 19.3 | 67,177 | 17.9 |
| Vyanzo Visivyohifadhiwa | 4,233,481 | 29.9 | 4,205,584 | 30.5 | 27,897 | 7.4 |
| **Aina ya Choo** | | | | | | |
| Choo cha Kuvuta | 4,921,712 | 34.8 | 4,700,459 | 34.1 | 221,253 | 58.9 |
| Choo cha Shimo Kilichoboreshwa (VIP) | 1,012,866 | 7.2 | 974,087 | 7.1 | 38,779 | 10.3 |
| Choo cha Shimo | 7,364,853 | 52.0 | 7,281,733 | 52.9 | 83,120.0 | 22.1 |
| Aina Nyingine ya Choo | 64,967 | 0.5 | 64,294 | 0.5 | 673 | 0.2 |
| Hakuna Choo | 788,405 | 5.6 | 756,402 | 5.5 | 32,003 | 8.5 |
| **Aina ya Utupaji Taka** | | | | | | |
| Zinakusanywa na Kampuni / Mamlaka | 3,501,041 | 24.7 | 3,347,772 | 24.3 | 153,269 | 40.8 |
| Zinachomwa | 5,672,185 | 40.1 | 5,575,075 | 40.5 | 97,110 | 25.8 |
| Zinatupwa pembezoni mwa Barabara | 69,409 | 0.5 | 67,618 | 0.5 | 1,791.0 | 0.5 |
| Zinafukiwa/Kutupwa kwenye Shimo | 2,898,583 | 20.5 | 2,874,416 | 20.9 | 24,167 | 6.4 |
| Sehemu nyingine (Porini, Sehemu za Wazi) | 2,011,585 | 14.2 | 1,912,094 | 13.9 | 99,491 | 26.5 |
| **Umiliki wa Mali (Assets)** | | | | | | |
| Jembe la Mkono | 7,790,461 | 55.0 | 7,637,583 | 55.4 | 152,878.0 | 40.7 |
| Ardhi/Shamba | 8,929,153 | 63.1 | 8,761,355 | 63.6 | 167,798 | 44.6 |
| Nyumba | 9,133,020 | 64.5 | 8,865,242 | 64.3 | 267,778 | 71.3 |
| Baiskeli | 3,014,581 | 21.3 | 2,900,736 | 21.1 | 113,845 | 30.3 |
| Pikipiki/Vespa | 1,147,195 | 8.1 | 1,093,775 | 7.9 | 53,420.0 | 14.2 |
| Trekta la Mkono (Power tiller) | 42,333 | 0.3 | 41,576 | 0.3 | 757 | 0.2 |
| Nyaraka za Utambulisho wa Kitaifa | | | | | | |
| Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa/Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (NHIF/CHIF) | 4,230,573 | 7.0 | 4,125,988 | 7.0 | 104,585 | 5.6 |
| Aina nyingine ya Bima ya Afya | 735,407 | 1.2 | 691,294 | 1.2 | 44,113 | 2.4 |
| Kitambulisho cha Taifa | 7,133,230 | 23.3 | 6,579,831 | 22.2 | 553,399 | 57.3 |
| Namba ya Kitambulisho cha Taifa | 4,119,156 | 13.4 | 4,080,447 | 13.7 | 38,709 | 4.0 |
| Kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi | 575,598 | 1.9 | 18,607 | 0.1 | 556,991 | 57.6 |
| Leseni ya Udereva | 1,399,993 | 4.6 | 1,298,607 | 4.4 | 101,386 | 10.6 |
| Kadi ya Mpiga Kura | 19,446,522 | 63.4 | 18,909,754 | 63.7 | 536,768 | 55.5 |
| Pasi ya Kusafiia | 637,325 | 1.1 | 562,058 | 1.0 | 75,267 | 4.1 |

## Muhtasari wa Matokeo Muhimu kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Asilimia ya Kaya Zinazoongozwa na Wanawake | Asilimia ya Wajane | Asilimia ya Watu wenye Vyeti vya Kuzaliwa | Asilimia ya Watoto Yatima | Asilimia ya Watu Wazima Wanaojua Kusoma na Kuandika | Uandikishaji Halisi Shule za Msingi | Kiwango cha Ulemavu | Asilimia ya Kaya Zinazotumia Nishati ya Umeme Kuangazia | Asilimia ya Kaya Zinazotumia Maji ya Bomba | Asilimia ya Kaya Zisizo na Vyoo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Wanaume | Wanawake | | | | | | | | | | |
| **Tanzania** | **61,741,120** | **30,053,130** | **31,687,990** | **35.8** | **4.7** | **28.8** | **10.4** | **83.0** | **83.3** | **11.2** | **37.4** | **50.9** | **5.6** |
| | | | | | | | | | | | | | |
| **Tanzania Bara** | **59,851,347** | **29,137,638** | **30,713,709** | **35.9** | **4.8** | **27.3** | **10.5** | **82.8** | **82.9** | **11.2** | **36.6** | **50.2** | **5.5** |
| Dodoma | 3,085,625 | 1,512,760 | 1,572,865 | 35.4 | 5.5 | 26.8 | 8.4 | 76.3 | 77.4 | 12.3 | 28.9 | 58.2 | 5.3 |
| Arusha | 2,356,255 | 1,125,616 | 1,230,639 | 40.7 | 4.1 | 35.7 | 9.6 | 84.8 | 85.0 | 9.8 | 52.3 | 79.7 | 15.3 |
| Kilimanjaro | 1,861,934 | 907,636 | 954,298 | 37.5 | 6.9 | 38.8 | 8.7 | 94.2 | 96.4 | 15.3 | 63.1 | 86.6 | 2.4 |
| Tanga | 2,615,597 | 1,275,665 | 1,339,932 | 35.6 | 6.0 | 26.2 | 8.5 | 83.0 | 86.2 | 10.4 | 33.5 | 49.5 | 7.3 |
| Morogoro | 3,197,104 | 1,579,869 | 1,617,235 | 32.6 | 4.8 | 25.6 | 10.1 | 82.1 | 81.9 | 12.1 | 33.4 | 54.1 | 4.2 |
| Pwani | 2,024,947 | 998,616 | 1,026,331 | 34.2 | 4.3 | 32.0 | 9.7 | 86.4 | 89.8 | 11.4 | 41.9 | 54.9 | 4.6 |
| Dar es Salaam | 5,383,728 | 2,600,018 | 2,783,710 | 33.9 | 3.3 | 52.3 | 8.6 | 97.5 | 96.8 | 11.2 | 86.0 | 79.5 | 0.2 |
| Lindi | 1,194,028 | 582,120 | 611,908 | 34.8 | 4.0 | 25.0 | 10.4 | 77.6 | 83.1 | 14.4 | 18.8 | 45.6 | 5.0 |
| Mtwara | 1,634,947 | 776,782 | 858,165 | 36.6 | 3.8 | 27.0 | 9.3 | 78.0 | 89.8 | 14.5 | 16.6 | 39.6 | 2.7 |
| Ruvuma | 1,848,794 | 902,298 | 946,496 | 30.7 | 4.1 | 20.9 | 9.3 | 86.6 | 88.1 | 10.9 | 24.8 | 51.5 | 1.4 |
| Iringa | 1,192,728 | 574,313 | 618,415 | 39.2 | 7.4 | 39.7 | 11.4 | 89.5 | 94.1 | 10.9 | 43.1 | 57.3 | 1.2 |
| Mbeya | 2,343,754 | 1,123,828 | 1,219,926 | 37.2 | 6.8 | 32.5 | 11.3 | 87.9 | 85.8 | 11.2 | 44.7 | 62.0 | 2.7 |
| Singida | 2,008,058 | 995,703 | 1,012,355 | 35.7 | 5.4 | 24.3 | 9.2 | 79.4 | 78.3 | 11.3 | 21.2 | 32.5 | 7.9 |
| Tabora | 3,391,679 | 1,661,171 | 1,730,508 | 35.0 | 4.0 | 15.1 | 11.6 | 68.0 | 63.4 | 9 | 20.2 | 22.1 | 13.6 |
| Rukwa | 1,540,519 | 743,119 | 797,400 | 35.3 | 4.5 | 13.6 | 10.0 | 74.1 | 72.1 | 9.3 | 19.5 | 37.0 | 3.8 |
| Kigoma | 2,470,967 | 1,186,833 | 1,284,134 | 35.8 | 5.0 | 11.5 | 18.8 | 76.7 | 81.6 | 11.4 | 17.7 | 32.8 | 3.4 |
| Shinyanga | 2,241,299 | 1,102,879 | 1,138,420 | 36.5 | 3.9 | 24.8 | 10.2 | 77.3 | 77.5 | 8.8 | 25.9 | 44.1 | 8.3 |
| Kagera | 2,989,299 | 1,459,280 | 1,530,019 | 33.9 | 5.4 | 14.3 | 10.5 | 80.1 | 83.5 | 12.8 | 21.3 | 28.6 | 2.5 |
| Mwanza | 3,699,872 | 1,802,183 | 1,897,689 | 38.7 | 4.4 | 24.0 | 10.2 | 85.6 | 89.1 | 11.8 | 37.7 | 51.0 | 3.9 |

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Asilimia ya Kaya Zinazoongozwa na Wanawake | Asilimia ya Wajane | Asilimia ya Watu wenye Vyeti vya Kuzaliwa | Asilimia ya Watoto Yatima | Asilimia ya Watu Wazima Wanaojua Kusoma na Kuandika | Uandikishaji Halisi Shule za Msingi | Kiwango cha Ulemavu | Asilimia ya Kaya Zinazotumia Nishati ya Umeme Kuangazia | Asilimia ya Kaya Zinazotumia Maji ya Bomba | Asilimia ya Kaya Zisizo na Vyoo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Wanaume | Wanawake | | | | | | | | | | |
| Mara | 2,372,015 | 1,139,511 | 1,232,504 | 42.3 | 6.4 | 31.4 | 12.6 | 85.9 | 91.2 | 12.1 | 26.1 | 25.3 | 15.3 |
| Manyara | 1,892,502 | 954,879 | 937,623 | 35.2 | 3.9 | 23.2 | 9.7 | 78.2 | 78.5 | 9.7 | 23.1 | 47.9 | 17.3 |
| Njombe | 889,946 | 420,533 | 469,413 | 39.5 | 7.5 | 35.1 | 10.6 | 90.0 | 95.5 | 10.7 | 35.9 | 62.4 | 0.4 |
| Katavi | 1,152,958 | 569,902 | 583,056 | 31.0 | 3.6 | 11.5 | 12.2 | 70.4 | 64.6 | 9.9 | 20.3 | 34.7 | 7.0 |
| Simiyu | 2,140,497 | 1,034,681 | 1,105,816 | 42.5 | 5.0 | 22.3 | 10.5 | 75.0 | 76.0 | 9.1 | 15.9 | 34.9 | 9.1 |
| Geita | 2,977,608 | 1,463,764 | 1,513,844 | 35.4 | 3.7 | 25.9 | 10.5 | 77.0 | 80.3 | 10.2 | 19.9 | 18.3 | 5.2 |
| Songwe | 1,344,687 | 643,679 | 701,008 | 36.2 | 5.5 | 27.7 | 9.6 | 81.0 | 81.0 | 10.5 | 28.1 | 28.1 | 2.9 |
| **Tanzania Zanzibar** | **1,889,773** | **915,492** | **974,281** | **30.7** | **3.0** | **75.1** | **6.4** | **90.6** | **96.9** | **11.4** | **66.9** | **74.7** | **8.5** |
| Kaskazini Unguja | 257,290 | 126,341 | 130,949 | 29.0 | 3.2 | 70.9 | 6.3 | 85.4 | 96.2 | 10.3 | 44.2 | 75.4 | 8.7 |
| Kusini Unguja | 195,873 | 98,367 | 97,506 | 29.2 | 2.5 | 74.0 | 6.9 | 93.9 | 97.8 | 11.6 | 54.0 | 67.3 | 5.5 |
| Mjini Magharibi | 893,169 | 427,927 | 465,242 | 29.8 | 2.7 | 81.1 | 6.2 | 96.2 | 98.2 | 10.8 | 88.9 | 73.5 | 0.3 |
| Kaskazini Pemba | 272,091 | 131,484 | 140,607 | 33.8 | 3.9 | 64.6 | 6.4 | 77.2 | 93.9 | 13.2 | 39.8 | 74.9 | 30.9 |
| Kusini Pemba | 271,350 | 131,373 | 139,977 | 34.2 | 3.4 | 70.6 | 6.4 | 85.2 | 96.7 | 12.1 | 48.8 | 85.5 | 19.8 |

# 2.0 Idadi na Ongezeko la Watu

## 2.1 Idadi ya Watu


Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 (SWM 2022) yanaonesha kuwa idadi ya watu Tanzania ni 61,741,120. Kati ya hao, wanaume ni 30,053,130 (48.7%) na wanawake ni 31,687,990 (51.3%). Asilimia 96.9 ya watu wote Tanzania wanaishi Tanzania Bara na asilimia 3.1 wanaishi Tanzania Zanzibar.

Idadi ya Watu Tanzania imeongezeka kwa asilimia 37.4 kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 hadi kufikia watu 61,741,120 mwaka 2022 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 30.4 katika kipindi cha mwaka 2002 mpaka 2012. Hali hii ya ongezeko inaonekana pia Tanzania Bara. Tanzania Zanzibar imekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu kutoka asilimia 32.8 katika kipindi cha 2002 - 2012 hadi kufikia asilimia 45.0 katika kipindi cha 2012 - 2022.

## 2.2 Kasi ya Ongezeko la Idadi ya Watu


Idadi ya watu Tanzania imeongezeka kwa wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka, kati ya mwaka 2012 na 2022. Kwa kasi hii ya ongezeko, idadi ya watu Tanzania inatarajiwa kuwa mara mbili ya idadi iliyopo sasa katika kipindi cha miaka 22 ijayo, yaani ifikapo mwaka 2044. Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka imeongezeka kutoka asilimia 2.7 katika kipindi cha 2002-2012 hadi kufikia asilimia 3.2 kwa kipindi cha 2012-2022.

**Wastani wa Kasi ya Ongezeko la Idadi ya Watu kwa Mwaka kwa Vipindi vya Sensa; Tanzania, SWM, 1967–2022**



Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi wa watu kwa mwaka katika kipindi cha 2012-2022 inatofautiana kati ya mkoa mmoja na mwingine. Mkoa wenye kasi ndogo ya ongezeko la idadi ya watu ni Kilimanjaro (1.3 %) na mkoa wenye kasi kubwa ya ongezeko ni Katavi (7.1%). Mikoa 13 ina kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka zaidi ya wastani wa kitaifa (3.2%).

**Wastani wa Kasi ya Ongezeko la Idadi wa Watu kwa Mwaka kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2012 - 2022**




## 3.0 Idadi ya Kaya

Matokeo ya SWM 2022 yanaonesha kuwa Tanzania ina kaya binafsi 14,152,803. Kati ya hizo, kaya 13,776,975 (97.3%) zipo Tanzania Bara na 378,828 (2.7%) zipo Tanzania Zanzibar. Idadi ya kaya Tanzania imeongezeka kutoka 9,362,758 mwaka 2012 hadi 14,152,803 mwaka 2022, ikiwa ni ongezeko la kaya 4,790,045 (51.2%).


Kati ya kaya zote binafsi nchini, asilimia 64.2 zinaongozwa na wanaume na asilimia 35.8 zinaongozwa na wanawake. Asilimia ya kaya zinazoongozwa na wanawake Tanzania Bara ni kubwa (35.9%) ikilinganishwa na Tanzania Zanzibar (30.7%). Kiwango hiki cha kaya zinazoongozwa na wanawake kimeongezeka kidogo kutoka asilimia 33.4 mwaka 2012 hadi asilimia 35.8 mwaka 2022.

**Asilimia ya Kaya Zinazoongozwa na Wanawake; Tanzania, SWM 2012 na 2022**




Mkoa wa Simiyu kwa Tanzania Bara, una kiwango kikubwa zaidi cha kaya zinazoongozwa na wanawake (42.5%) na Mkoa wa Ruvuma una kiwango kidogo zaidi (30.7%). Kwa Tanzania Zanzibar, kiwango cha kaya zinazoongozwa na wanawake ni kutoka asilimia 29.0 kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja hadi asilimia 34.2 Mkoa wa Kusini Pemba.


**Asilimia ya Kaya Zinazoongozwa na Wanawake kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 4.0 Idadi ya Watu katika Kaya

Wastani wa idadi ya watu katika kaya umepungua kutoka watu 4.8 mwaka 2012 hadi watu 4.3 mwaka 2022 kwa Tanzania na Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, wastani wa idadi ya watu katika kaya umepungua kutoka watu 5.1 mwaka 2012 hadi watu 4.9 mwaka 2022. Wastani wa idadi ya watu katika kaya unatofautiana kimkoa kutoka watu 3.3 kwa Mkoa wa Mtwara hadi watu 6.7 kwa Mkoa wa Simiyu.


**Wastani wa Idadi ya Watu katika Kaya kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 5.0 Hali ya Ndoa


Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa, asilimia 51.4 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi Tanzania wameoa au kuolewa na asilimia 5.5 wanaishi pamoja. Asilimia ya wanawake walioolewa au kuishi pamoja ni kubwa (52.4%) ikilinganishwa na wanaume waliooa au kuishi pamoja (50.3%). Takriban asilimia tano (4.7%) ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi ni wajane, ambapo asilimia ya wajane ni kubwa (7.9%) ikilinganishwa na ya wagane (1.3%).

**Asilimia ya Mgawanyo wa Watu wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi kwa Hali ya Ndoa; Tanzania, SWM 2022**




Matokeo yanaonesha kuwa asilimia ya watu waliooa au kuolewa (51.4%) haikubadilika sana ikilinganishwa na sensa ya mwaka 2012 (51.1%). Asilimia ya watu walioachana imeongezeka kutoka asilimia 0.9 mwaka 2012 mpaka asilimia 3.7 mwaka 2022, na asilimia ya wajane imeongezeka kutoka 3.1 mpaka 4.7 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.


**Asilimia ya Mgawanyo wa Watu wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi kwa Hali ya Ndoa; Tanzania, SWM 2012 na 2022**




## 5.1 Wastani wa Umri wa Kuoa au Kuolewa kwa Mara ya Kwanza


Matokeo ya SWM 2022, yanaonesha kuwa umri wa wastani wa kuoa au kuolewa kwa mara ya kwanza ni miaka 24.1, ambapo wanawake wanaolewa wakiwa na wastani wa miaka 22.1 na wanaume wanaoa wakiwa na wastani wa miaka 26.4. Matokeo yanaonesha wastani wa umri wa kuolewa kwa wanawake kwa mara ya kwanza umepungua kidogo kutoka miaka 22.3 mwaka 2012 hadi miaka 22.1 mwaka 2022 ambapo wastani wa umri wa kuoa umeongezeka kutoka miaka 25.8 kwa mwaka 2012 hadi miaka 26.4 mwaka 2022.

**Wastani wa Umri wa Kuoa au Kuolewa kwa Mara ya Kwanza kwa Jinsi; Tanzania, SWM 2012 na 2022**



Wastani wa umri wa kuoa au kuolewa kwa mara ya kwanza unatofautiana kimkoa. Mkoa wenye wastani mkubwa wa umri wa kuoa/kuolewa kwa mara ya kwanza ni Mkoa wa Dar es Salaam (miaka 29.2 kwa wanaume na miaka 25.7 kwa wanawake), ukifuatiwa na Mkoa wa Kilimanjaro (wanaume miaka 29.0 na miaka 24.5 kwa wanawake). Mikoa yenye wastani mdogo wa umri wa kuolewa kwa mara ya kwanza ni Mkoa wa Katavi (miaka 21.8) na wastani mdogo wa umri wa kuoa ni Mkoa wa Rukwa (miaka 22.0).


**Wastani wa Umri wa Kuoa au Kuolewa kwa Mara ya Kwanza kwa Jinsi na Mkoa; Tanzania, SWM 2012 na 2022**



## 6.0 Vyeti vya Kuzaliwa


Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa asilimia 28.8 ya watu wote Tanzania wana vyeti vya kuzaliwa, ambapo asilimia 3.1 walikuwa na tangazo la kizazi. Asilimia ya watu wenye vyeti vya kuzaliwa ni kubwa (75.1%) kwa Tanzania Zanzibar ikilinganishwa na Tanzania Bara (27.3%). Aidha, asilimia 4.3 ya watu Tanzania Zanzibar wana tangazo la kizazi ikilinganishwa na asilimia 3.0 kwa Tanzania Bara.

**Asilimia ya Mgawanyo wa Watu kwa Hali ya Umiliki wa Vyeti vya Kuzaliwa; Tanzania, SWM 2022**




Mikoa ya Tanzania Zanzibar ina asilimia kubwa ya watu wenye vyeti vya kuzaliwa ikilinganishwa na Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, mkoa wenye asilimia kubwa ya watu wenye vyeti vya kuzaliwa ni Mjini Magharibi (81.1%) ambapo Mkoa Kaskazini Pemba una kiwango cha chini (64.6%). Kwa Tanzania Bara, mkoa wenye asilimia kubwa ya watu wenye vyeti vya kuzaliwa ni Dar es Salaam (52.3%) na mikoa yenye kiwango cha chini ni Katavi na Kigoma (11.5% kila mmoja).


**Asilimia ya Watu Wenye Vyeti vya Kuzaliwa kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 7.0 Vitambulisho vya Taifa

Asilimia 23.3 ya watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi Tanzania wana vitambulisho vya taifa ambapo asilimia 13.4 wana namba za kitambulisho cha taifa pekee na asilimia 63.4 wana kitambulisho cha mpiga kura. Tanzania Bara ina asilimia 22.2 ya watu wenye kitambulisho cha taifa na asilimia 13.7 wana namba za kitambulisho cha taifa na asilimia 63.7 wana kitambulisho cha mpiga kura . Kwa Tanzania Zanzibar, zaidi ya nusu (57.3%) ya watu wana kitambulisho cha taifa ambapo asilimia 4.0 wana namba za kitambulisho cha taifa na asilimia 55.5 wana kitambulisho cha mpiga kura. Aidha, asilimia 57.6 ya watu Tanzania Zanzibar wana vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi.

**Asilimia ya Watu Wanaomiliki Vitambulisho vya Taifa; Tanzania, SWM 2022**




## 8.0 Bima ya Afya

Asilimia saba ya watu Tanzania wana bima ya afya kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) au Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHIF) na asilimia 1.2 wana bima ya afya kutoka kwenye taasisi nyingine zinazotoa huduma hiyo. Kwa Tanzania Bara, asilimia 7.0 ya watu wana bima ya afya kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) au Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHIF) ambapo kwa Tanzania Zanzibar ni asilimia 5.6.


Mkoa wa Dar es Salaam kwa Tanzania Bara una asilimia kubwa (14.8%) ya watu wenye bima ya NHIF/CHIF ukifuatiwa na Mkoa wa Kilimanjaro (12.2%). Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi una asilimia kubwa (8.4%) ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Unguja (4.5%).

**Asilimia ya Watu Wenye Bima ya Afya ya Taifa (NHIF/CHIF) kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**




Matokeo yanaonesha kuwa, asilimia 13.8 ya watu wenye umri wa miaka 60 na zaidi wana kadi ya matibabu kwa wazee. Kwa Tanzania Bara, asilimia 14.0 wana kadi ya matibabu kwa wazee ambapo Tanzania Zanzibar ni asilimia 4.5. Asilimia ya wanawake walio na kadi za matibabu kwa wazee ni kubwa (14.2%) ikilinganishwa ile ya wanaume (13.3%).


**Asilimia ya Watu Wenye Miaka 60 na Zaidi Walio na Kadi ya Matibabu kwa Wazee; Tanzania, SWM 2022**




## 9.0 Hali ya Uyatima

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 10.4 ya watoto chini ya miaka 18 Tanzania ni yatima. Kati yao, asilimia 5.2 wamefiwa na baba peke yake, 1.8 wamefiwa na mama peke yake, na asilimia 3.4 wamefiwa na wazazi wote wawili. Asilimia ya watoto yatima ni kubwa Tanzania Bara (10.5%) ikilinganishwa na Tanzania Zanzibar (6.4%).

**Hali ya Uyatima; Tanzania, SWM 2022**





## 10.0 Kiwango cha Kujua Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima

Matokeo yanaonesha kuwa, asilimia 83.0 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi Tanzania wanajua kusoma na kuandika. Kiwango cha kujua kusoma na kuandika kwa Tanzania Bara ni karibu sawa na kile cha Tanzania. Hata hivyo, kiwango cha kujua kusoma na kuandika ni kikubwa (90.6%) kwa Tanzania Zanzibar ikilinganishwa na kile


cha Tanzania Bara (82.8%). Kiwango cha kujua kusoma na kuandika ni kikubwa (86.8%) kwa wanaume ikilinganishwa na wanawake (79.5%).

**Kiwango cha Kujua Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima (Miaka 15 na Zaidi) kwa Jinsi; Tanzania, SWM 2022**





Kiwango cha kujua kusoma na kuandika kwa watu wazima kimeongezeka kutoka asilimia 78.1 mwaka 2012 hadi asilimia 83.0 mwaka 2022. Hali kama hii imeonekana kwa wanaume na wanawake.

**Kiwango cha Kujua Kusoma na Kuandika kwa Watu wazima (Miaka 15 na Zaidi) kwa Jinsi; Tanzania, SWMT 2012 na 2022**




Kiwango cha kujua kusoma na kuandika kwa watu wazima kinatofautiana kimkoa kutoka asilimia 68.0 kwa Mkoa wa Tabora hadi asilimia 97.5 kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Mikoa mingine yenye kiwango cha kujua kusoma na kuandika kinachozidi asilimia 90 ni Mjini Magharibi (96.2%), Kilimanjaro (94.2%) na Kusini Unguja (93.9%). Mikoa mingine yenye kiwango kidogo cha kujua kusoma na kuandika ni Katavi (70.4%), Rukwa (74.1%) na Simiyu (75.0%).


**Kiwango cha Kujua Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima (Miaka 15 na Zaidi) kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 11.0 Kiwango Halisi cha Uandikishaji


Kiwango Halisi cha Uandikishaji (Net Enrolment Rate) katika shule za msingi Tanzania ni asilimia 83.3; kiwango hiki ni kikubwa kwa wanawake (85.4 %) ikilinganishwa na wanaume (81.2%). Matokeo pia yanaonesha kuwa, kiwango halisi cha uandikishaji katika shule za msingi ni kikubwa kwa Tanzania Zanzibar (96.9%) ikilinganishwa na asilimia 82.9 kwa Tanzania Bara.

**Kiwango Halisi cha Uandikishaji Shule za Msingi (Miaka 7-13) kwa Jinsi; Tanzania, SWM 2022**





Kiwango Halisi cha Uandikishaji Tanzania kimeongezeka kutoka asilimia 76.8 mwaka 2012 hadi asilimia 83.3 mwaka 2022. Kiwango kama hicho pia kimeonekana kwa Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, Kiwango Halisi cha Uandikishaji kimeongezeka kutoka asilimia 85.9 mwaka 2012 hadi asilimia 96.9 mwaka 2022.

**Kiwango Halisi cha Uandikishaji katika Shule za Msingi (Miaka 7-13); Tanzania, SWM 2012 na 2022**



Matokeo yanaonesha kuwa Mkoa wa Kilimanjaro kwa Tanzania Bara una kiwango kikubwa (96.4%) cha uandikishaji halisi ambapo Mkoa wa Tabora una kiwango kidogo (63.4%). Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi una kiwango kikubwa cha uandikishaji halisi (98.2%) ambapo Mkoa wa Kaskazini Pemba una kiwango kidogo (93.9%).


**Kiwango Halisi cha Uandikishaji katika Shule za Msingi (Miaka 7-13) kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 12.0 Hali ya Mahudhurio Shuleni

Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa, kati ya watu wenye umri wa miaka minne na zaidi Tanzania, asilimia 19.9 hawajawahi kuhudhuria shule; kiwango ni kikubwa zaidi (21.8%) kwa wanawake ikilinganishwa na wanaume (17.9%). Kiwango cha kutohudhuria shule ni kikubwa (20.2%) kwa Tanzania Bara ikilinganishwa na Tanzania Zanzibar (11.2%).


**Asilimia ya Mgawanyo wa Watu wenye Umri wa Miaka Minne na Zaidi kwa Jinsi na Hali ya Mahudhurio Shuleni; Tanzania SWM 2022**




## 13.0 Hali ya Kazi katika Ajira

Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa watu wengi waliokatika ajira (43.2%) wanajishughulisha na kazi za kilimo/uvuvi ikifuatiwa na wale walio katika kazi ya kawaida zisizo za ujuzi (21.7%), na kazi za ufundi wa kutumia mikono (19.7%). Hali kama hii imeonekana kwa Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, idadi kubwa ya watu walioajiriwa (27.3%) wako katika kazi za kawaida zisizo za ujuzi ikifuatiwa na kilimo/uvuvi (24.2%).

**Asilimia ya Mgawanyo wa Watu Wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi Walioajiriwa kwa Aina ya Kazi; Tanzania, SWM 2022**





## 14.0 Kiwango cha Ulemavu

Matokeo ya Sensa 2022, yanaonesha kuwa asilimia 11.2 ya watu Tanzania, wenye umri wa miaka 7 na zaidi wana aina fulani ya ulemavu. Kuna tofauti ndogo ya kiwango cha watu wenye ulemavu kati ya Tanzania Bara (11.2%) na Tanzania Zanzibar (11.4%).

Kiwango cha ulemavu kinatofautiana kati ya mkoa na mkoa. Mkoa wa Shinyanga una kiwango kidogo (8.8%) ya watu wenye ulemavu ambapo Mkoa wa Kilimanjaro una kiwango kikubwa (15.3%).


**Kiwango cha Ulemavu kwa Watu wenye Umri wa Miaka 7 na Zaidi kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**


Kilimanjaro 15.3
Mtwara 14.5
Lindi 14.4
Kaskazini Pemba 13.2
Kagera 12.8
Dodoma 12.3
Kusini Pemba 12.1
Mara 12.1
Morogoro 12.1
Mwanza 11.8
Kusini Unguja 11.6
Kigoma 11.4
Pwani 11.4
Singida 11.3
Mbeya 11.2
Dar es Salaam 11.2
Iringa 10.9
Ruvuma 10.9
Mjini Magharibi 10.8
Njombe 10.7
Songwe 10.5
Tanga 10.4
Kaskazini Unguja 10.3
Geita 10.2
Katavi 9.9
Arusha 9.8
Manyara 9.7
Rukwa 9.3
Simiyu 9.1
Tabora 9.0
Shinyanga 8.8
Tanzania Zanzibar 11.4
Tanzania Bara 11.2
Tanzania 11.2

## 15.0 Hali ya Umiliki wa Ardhi


Asilimia 32.5 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi Tanzania wanamiliki ardhi ambapo asilimia 29.2 ya wanawake wanamiliki ardhi ikilinganishwa na asilimia 36.2 ya wanaume. Umiliki wa ardhi kwa Tanzania Bara ni asilimia 33.0 na Tanzania Zanzibar ni asilimia 16.2.

**Mgawanyo wa Asilimia ya Watu wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi Wanaomiliki Ardhi kwa Jinsi; Tanzania, SWM 2022**




Matokeo yanaonesha kuwa, kwa Tanzania Bara, Mkoa wa Mtwara una asilimia kubwa (47.0%) ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanaomiliki ardhi ukifuatiwa na Mkoa wa Ruvuma (45.3%). Aidha, Mikoa ya Dar es Salaam na Katavi ina asilimia ndogo ya watu wanaomiliki ardhi (21.2% na 23.0% mtawalia). Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Kaskazini Unguja una asilimia ndogo ya watu wanaomiliki ardhi (12.6%) na Mkoa wa Kusini Unguja una asilimia kubwa (22.9%).


**Asilimia ya Watu Wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi Wanaomiliki Ardhi kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 16.0 Umiliki wa Rasilimali (Assets) katika Kaya

Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa, asilimia 64.5 ya kaya Tanzania zinamiliki nyumba. Asilimia ya kaya zinazomiliki nyumba ni kubwa (71.3%) kwa Tanzania Zanzibar ikilinganishwa na Tanzania Bara (64.3%). Matokeo pia yanaonesha kuwa, asilimia 63.1 ya kaya Tanzania zinamiliki ardhi au shamba na asilimia 55.0 zinamiliki jembe la mkono.


**Asilimia ya Umilikaji wa Rasilimali katika Kaya; Tanzania, SWM 2022**



## 17. Kaya Zinazotumia Nishati ya Umeme Kuangazia


Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa asilimia 37.4 ya kaya Tanzania zinatumia umeme wa gridi ya Taifa (TANESCO/ZECO) kama chanzo kikuu cha nishati ya kuangazia. Matumizi ya umeme kama chanzo kikuu cha nishati ya kuangazia kwa Tanzania Zanzibar ni makubwa (66.9%) ikilinganishwa na Tanzania Bara (36.6%). Aidha, Mkoa wa Simiyu una kiwango cha chini zaidi cha kaya (15.9%) zinazotumia umeme kama chanzo kikuu cha nishati ya kuangazia ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi una kiwango cha juu zaidi (88.9%).

**Asilimia ya Kaya Zinazotumia Umeme kutoka Gridi ya Taifa kama Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**




Asilimia ya kaya zinazotumia umeme wa gridi ya Taifa kwa kuangazia Tanzania imeongezeka kutoka asilimia 21.3 mwaka 2012 hadi asilimia 37.4 mwaka 2022. Kwa Tanzania Bara, ongezeko hilo ni kutoka asilimia 20.7 hadi 36.6 na kwa Tanzania Zanzibar asilimia 42.9 hadi asilimia 66.9.

**Asilimia ya Kaya Zinazotumia Umeme kutoka Gridi ya Taifa Kama Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia Tanzania; SWMT 2012 na 2022**





## 18.0 Kaya zinazotumia Maji ya Bomba/Mfereji

Matokeo ya Sensa 2022 yanaonyesha kuwa, karibu nusu ya kaya zote Tanzania na Tanzania Bara (50.9% na 50.2% mtawalia) zinatumia maji ya bomba/mfereji kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa. Hata hivyo, kwa Tanzania Zanzibar takriban robo tatu (74.7%) ya kaya zote zinatumia maji ya bomba/mfereji kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa.


Aidha, kaya zinazotumia maji ya bomba/mfereji kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa kwa Tanzania zimeongezeka kutoka asilimia 37.0 mwaka 2012 hadi asilimia 50.9 mwaka 2022. Kwa Tanzania Bara, ongezeko hilo ni kutoka asilimia 36.0 hadi 50.2 na asilimia 73.0 hadi 74.7 kwa Tanzania Zanzibar.

**Asilimia ya Kaya Zinazotumia Maji ya Bomba/Mfereji Kama Chanzo Kikuu cha Maji ya Kunywa; Tanzania, SWM 2012 na 2022**



Matumizi ya maji ya bomba/mfereji kama chanzo kikuu cha maji ya kunywa kwa kaya yanatofautiana kimkoa kuanzia asilimia 18.3 kwa Mkoa wa Geita hadi asilimia 86.6 kwa Mkoa Kilimanjaro.

**Asilimia ya Kaya Zinazotumia Maji ya Bomba/Mfereji kama Chanzo Kikuu cha Maji ya Kunywa kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**




**Maji ya Bomba**



Tanzania: 50.9%


Tanzania Bara: 50.2%

Tanzania Zanzibar: 74.7%

## 19.0 Kaya zisizo na Vyoo


Matokeo ya Sensa 2022, yanaonesha kuwa asilimia 5.6 ya kaya Tanzania hazina vyoo. Asilimia ya kaya zisizo na vyoo kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni 5.5 na 8.5 mtawalia. Aidha, asilimia ya kaya zisizo na vyoo inatofautiana kimkoa kutoka asilimia 0.2 kwa Dar es Salaam hadi asilimia 30.9 Kaskazini Pemba.

**Asilimia ya Kaya zisizo na Vyoo kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**




Hata hivyo, kaya zisizo na vyoo Tanzania zimepungua kutoka asilimia 7.8 mwaka 2012 hadi asilimia 5.6 mwaka 2022. Kwa Tanzania Bara, zimepungua kutoka asilimia 7.5 hadi 5.5 na Tanzania Zanzibar kutoka asilimia 19.3 hadi 8.5.


**Asilimia ya Kaya Zisizo na Vyoo; Tanzania, SWM 2012 na 2022**




## 20.0 Utupaji wa Taka Ngumu

Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa, asilimia 40.1 ya kaya zinachoma taka ngumu kama njia kuu ya utupaji taka ngumu ikifuatiwa na asilimia 21.9 ya kaya zinazotumia njia ya ukusanyaji wa mara kwa mara. Asilimia 40.5 ya kaya za Tanzania Bara, zinachoma taka ngumu kama njia kuu ya kutupa taka, ambapo kwa Tanzania Zanzibar asilimia 37.5 ya kaya zinatumia njia ya ukusanyaji wa mara kwa mara kama njia kuu. Utupaji wa taka ngumu kwa kutumia njia ya ukusanyaji wa mara kwa mara inatumika zaidi katika mikoa ya Dar es Salaam (64.4%) na Mjini Magharibi (asilimia 64.2).


**Asilimia ya Kaya kwa Aina ya Utupaji wa Taka Ngumu na Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



## 21.0 Umiliki Binafsi wa Simu za Mkononi


Matokeo ya Sensa 2022 yanaonesha kuwa, asilimia 82.5 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanamiliki simu ya mkononi. Kiwango cha watu wanaomiliki simu ya mkononi ni kikubwa zaidi kwa Tanzania Zanzibar (88.8%) ikilinganishwa na Tanzania Bara (82.3%). Umiliki wa simu ya mkononi ni mkubwa zaidi kwa wanaume ikilinganishwa na wanawake kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

**Asilimia ya Watu Wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi Wanaomiliki Simu ya Mkononikwa Jinsi; Tanzania, SWM 2022**





Umiliki wa simu ya mkononi (simu janja na simu za kawaida) unaongezeka kwa kasi baada ya umri wa miaka 14. Umiliki wa simu za kawaida uko kwa kiwango cha juu kwa watu wenye umri wa miaka 45-49 na 55-59 (asilimia 90.9 kwa kila kundi) na wanaomiliki simu njanja kiwango cha juu (asilimia 29.0) kiko kwa watu wenye umri wa miaka 25-29.

**Asilimia ya Watu Wenye Umri wa Miaka minne na Zaidi Wanaomiliki Simu ya Mkononi kwa Aina ya Simu na Umri; Tanzania, SWM 2022**




Mikoa yenye zaidi ya asilimia 90 ya watu wanaomiliki simu ya mkononi ni Dar es alaam (94.0%) ikifuatiwa na Mjini Magharibi (92.2%) na Kusini Unguja (91.8%). Mkoa wa Rukwa pekee una chini ya asilimia 75 ya watu wanaomiliki simu za mkononi (72.1%).

**Asilimia ya Watu Wenye Umri wa Miaka 15 au Zaidi Wanaomiliki Simu ya Mkononi kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022**



Dar es Salaam
94.0
Mjini Magharibi
92.2
Kusini Unguja
91.8
Kilimanjaro
89.4
Arusha
88.4
Pwani
87.2
Mbeya
86.4
Kaskazini Unguja
86.1
Njombe
85.2
Iringa
85.2
Tanga
84.0
Kusini Pemba
83.0
Morogoro
82.5
Songwe
82.3
Manyara
82.2
Dodoma
81.9
Kaskazini Pemba
81.8
Mwanza
81.6
Ruvuma
80.7
Lindi
80.3
Singida
78.8
Mara
78.3
Mtwara
78.2
Geita
77.6
Kagera
77.6
Kigoma
77.4
Shinyanga
76.6
Simiyu
75.4
Katavi
75.3
Tabora
75.2
Rukwa
72.1
Tanzania Zanzibar
88.8
Tanzania Bara
82.3
Tanzania
82.5

## 22.0 Umiliki wa Simu ya Mkononi katika Kaya

Asilimia 85.3 ya kaya Tanzania zina angalau mwanakaya mmoja mwenye umri wa miaka minne na zaidi ambaye anamiliki aina yoyote ya simu ya mkononi. Kiwango cha kaya zinazomiliki simu ya mkononi ni kikubwa (95.5%) kwa Tanzania Zanzibar ikilinganishwa na Tanzania Bara (85.0%).

Kiwango cha kaya zenye angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi Tanzania ni kati ya asilimia 69.4 kwa Mkoa wa Rukwa hadi asilimia 97.9 kwa Mkoa wa Mjini Magharibi. Mikoa yote ya Tanzania Zanzibar ina zaidi ya asilimia 90 ya kaya zenye angalau mwanakaya mmoja mwenye miaka minne na zaidi ambaye anamiliki simu ya mkononi.

**Asilimia ya Kaya Zenye Angalau Mwanakaya Mmoja Mwenye Umri wa Miaka Minne na Zaidi Anayemiliki Simu ya Mkononi kwa Mkoa; Tanzania, SWM 2022.**









Tanzania: 85.3%

Tanzania Bara: 85.0%

Tanzania Zanzibar: 95.5%

## 23.0 Umiliki Binafsi wa Kompyuta

Takriban asilimia nne (3.7%) ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi Tanzania wanamiliki kompyuta (asilimia 2.6 wanamiliki kompyuta mpakato na asilimia 1.1 wanamiliki kompyuta ya mezani). Asilimia ya watu wanaomiliki kompyuta Tanzania Zanzibar ni kubwa (5.6%) ikilinganishwa na ile ya Tanzania Bara (3.7%). Mkoa wa Dar es Salaam una asilimia kubwa ya watu wanaomiliki kompyuta (9.8%), ukifuatiwa na mikoa ya Mjini Magharibi (8.3%) na Arusha (5.9%).

**Asilimia ya Watu wenye Umri wa Miaka 15 na Zaidi Wanaomiliki Kompyuta kwa Mkoa; Tanzania, 2022 SWM**

